# KARATASI YA UKWELI
# Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa NSW

## Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa NSW ni nani?

Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa New South Wales ni DK James Cockayne. Muda wa miaka mitano wa Dk Cockayne ulianza tarehe 1 Agosti 2022.

Jukumu la Kamishna wa Kupambana na Utumwa liliundwa na *Modern Slavery Act 2018 (NSW) (Sheria ya Utumwa wa Kisasa ya 2018 (NSW))*. Inampa Kamishna majukumu ya:

- kutetea na kukuza hatua za kupambana na utumwa wa kisasa
- kutambua, na kutoa msaada na usaidizi kwa wahasiriwa wa utumwa wa kisasa
- kuhakikisha sheria na sera (policies) za serikali za kupambana na utumwa wa kisasa zinafanya kazi vizuri
- kusaidia na kusimamia juhudi za ununuzi wa umma za NSW ili kuondoa bidhaa za utumwa wa kisasa kutoka katika njia za usambazaji
- kutoa kanuni za utendaji na kudumisha rejesta ya umma inayohusiana na juhudi za kushughulikia hatari za utumwa wa kisasa katika njia za usambazaji
- kuongeza ufahamu wa jamii juu ya utumwa wa kisasa.

Office of the
NSW Anti-slavery
Commissioner

Working together
for real freedom

NSW Anti-slavery Commissioner's
Strategic Plan 2023–2026

## Utumwa wa kisasa ni nini?

Utumwa wa kisasa hutokea wakati mtu anapomtendea mtu mwingine kama kwamba ndiye anayemmiliki – kuzuia uhuru wake. Utumwa wa kisasa ni neno linalojumuisha aina mbalimbali za makosa ya kisheria. Hizi ni pamoja na:

- Utumwa
- Utumishi
- Utumwa wa ngono
- Kazi ya kulazimishwa
- Ndoa ya kulazimishwa
- Utumwa wa deni
- Usafirishaji haramu wa watu
- Kuajiri kwa udanganyifu kwa kazi au huduma
- Usafirishaji wa viungo na tishu
- Unyonyaji wa watoto kingono mtandaoni

## Je, kuna utumwa wa kisasa katika NSW?

Ndiyo. Kuna wastani wa watu milioni 50 wanaoishi katika utumwa wa kisasa duniani kote. Takriban watu 41,000 wanaishi katika utumwa wa kisasa nchini Australia, na inakadiriwa kuwa 16,400 huko New South Wales.

## Ni ipi baadhi ya mifano ya utumwa wa kisasa katika NSW?

Ofisi ya Kamishna wa Kupambana na Utumwa imepokea ripoti za kuaminika za aina nyingi tofauti za utumwa wa kisasa katika NSW, zikiwemo:

- Wafanyakazi walionaswa katika kazi ya kulazimishwa kwenye mashamba ya NSW ya kikanda (regional NSW).
- Wafanyakazi wanaolazimishwa katika utumwa wa nyumbani katika kaya za mijini.
- Wanawake na watoto, ambao wamefundishwa na kulazimishwa katika unyonyaji wa kingono, ana kwa ana na kupitia majukwaa (platforms) ya mitandao ya kijamii.
- Wasafishaji na walinzi wanaofanya kazi katika majengo ya ofisi, ambao wameshikwa katika utumwa wa madeni.
- Vijana wa kiume, wa kike na wasichana waliolazimishwa kuolewa hapa au nje ya nchi.
- Watu wanaoishi na ulemavu ambao wananyonywa katika maeneo ya kazi yaliyotengwa au katika uangalizi wa kitaasisi (institutional care).
- Kazi ya kulazimishwa na kazi ya watoto ya kulazimishwa ya watu wa Mataifa ya Kwanza.

# KARATASI YA UKWELI
# Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa NSW

## Je, Kamishna wa Kupambana na Utumwa anafanya nini kukomesha utumwa wa kisasa katika NSW?

Kamishna wa Kupambana na Utumwa anafanya ifuatayo:

**Kujenga uwezo wa kuzuia** – kufanya kazi na serikali ya NSW na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuwasaidia kutambua watu walio katika hatari ya utumwa wa kisasa na kuzuia unyanyasaji. Hii inahusisha kuandaa wafanyakazi walio mstari wa mbele na kuanzisha usaidizi madhubuti na nambari ya simu ya rufaa.

**Uwezeshaji wa tiba** – kufanya kazi na watoa huduma ili kuboresha ufikiaji kwa watu walio na uzoefu wa kuishi wa utumwa wa kisasa kupata tiba bora. Hii ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa usaidizi madhubuti na kukuza uongozi wa walionusurika.

**Kukuza mazoea ya kuwajibika ya biashara** – kufanya kazi na serikali na makampuni ya kibinafsi ili kuonyesha uongozi katika kutambua na kushughulikia utumwa wa kisasa katika njia ya usambazaji na uwekezaji. Hii ni pamoja na kuondoa bidhaa za utumwa wa kisasa kutoka kwa ununuzi wa umma na kukuza mazoea ya kuwajibika ya biashara katika sekta ya kibinafsi.

**Kubadilisha masimulizi** – kukuza ufahamu kuhusu utumwa wa kisasa kote katika NSW kwa njia ambayo inawawezesha waathirika na kujenga kesi za biashara na sera za kupinga utumwa.

**Kukuza jumuiya yenye malengo** – kuweka misingi ya utekelezaji endelevu na kushimika kunako shirikisha kwa *Modern Slavery Act 2018 (NSW) (Sheria ya Utumwa wa Kisasa ya 2018 (NSW))*, kuwaleta wadau pamoja ili kufanya kazi kufikia malengo ya Sheria hiyo na kuhakikisha kuwa juhudi za kupambana na utumwa wa kisasa zinaweza kuwa endelevu na zenye mafanikio.



## Je, wewe, au kuna mtu unayemjua, yuko hatarini?

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko ndani, au yuko katika hatari ya usafirishaji haramu wa binadamu au utumwa unaweza kuwasiliana na:

- Ofisi ya Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa NSW kwa antislavery@justice.nsw.gov.au. Tutakusaidia kukuelekeza kwenye huduma za usalama na usaidizi unazohitaji, kama vile malazi, ushauri wa kisheria na uhamiaji, ushauri na usaidizi wa kifedha. Kamishna wa Kupambana na Utumwa hatakiwi kutoa taarifa za ripoti iliyoshirikiwa naye, isipokuwa kama kuna sababu nzuri za kuwazia mtoto au kijana yuko katika hatari ya madhara makubwa; au
- Australian Federal Police (AFP) (Polisi la Kitaifa la Australia (AFP)) kwa 131 237 (131AFP) au nenda kwenye tovuti ya AFP katika www.afp.gov.au kwa usaidizi.

## Je, unahitaji mkalimani?

Ufafanuzi wa bure na wa siri unapatikana kwenye Translating & Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani) kwa nambari ya simu 131 450. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi ushauri nasaha. Simu zote ni za bure na za siri.

## Endelea kuwasiliana na Ofisi ya Kamishna wa Kupambana na Utumwa wa NSW

**Tembelea tovuti yetu**

**Website:** dcjnsw.info/antislaverycommissioner

**Facebook:** @Office of the NSW Anti-slavery Commissioner

**LinkedIn:** @Office of the NSW Anti-slavery Commissioner